JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TUME YA UTUMISHI WA UMMA

MWONGOZO KUHUSU UKIMWI NA KUWAHUDUMIA WATUMISHI WA TUME WANAOISHI NA VIRUSI VYA UKIMWI NA UKIMWI

Tolea Namba 1, Mwaka 2009.

DIBAJI

Mwongozo huu kuhusu UKIMWI na Kuwahudumia Watumishi wa Tume Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI na UKIMWI umeandaliwa ili kutoa maelekezo kwa watumishi wa Tume ya Utumishi wa Umma namna ambavyo Tume itawahudumia kabla ya kupata maambukizi na baada ya kupata maabukizi ya UKIMWI.

Mwongozo huu inaainisha huduma mbalimbali zitakazokuwa zinatolewa kwa watumishi wa Tume ya Utumishi wa Umma. Aidha, Mwongo huu pia umeonyesha majukumu ya watumishi ya kuyafanya ili wapate huduma hizo.

Ni matumaini ya Tume ya Utumishi wa Umma kuwa watumishi wa Tume ya Utumishi wa Umma kuwa watauzingatia kwa ukamilifu Mwongozo huu ili Tume iweze kuwahudumia ipasavyo katika kudhibiti UKIMWI ndani ya Tume.

Mwongozo huu utaanza kutumika tarehe 1 Februari, 2009.

Thecla W. Shangali
KATIBU
TUME YA UTUMISHI WA UMMA.

MWONGOZO KUHUSU UKIMWI NA KUWAHUDUMIA WATUMISHI WA TUME WANAOISHI NA VIRUSI VYA UKIMWI NA UKIMWI

1.0 UTANGULIZI

1.1 Kutangazwa kwa Janga la UKIMWI

Serikali ilitangaza ugonjwa wa UKIMWI kuwa ni janga la Kitaifa mwaka 1999. Hii ilitokana na ongezeko la upotevu wa nguvukazi pamoja na gharama kubwa ya matibabu ya wagonjwa wanaougua UKIMWI na huduma za kusafirisha maiti na mazishi.

1.2 Sera na Mkakati wa Kitaifa wa Kudhibiti UKIMWI

Serikali iliona umuhimu wa kuwepo kwa Sera ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI. Mnamo mwaka 2001 Sera ya Kudhibiti UKIMWI ilizinduliwa rasmi mkoani Dodoma. Aidha Katika juhudi za kutekeleza Sera ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI Serikali iliweka Mkakati wa Kitaifa wa kudhibiti UKIMWI ambao ulizinduliwa rasmi mwaka 2003 ambapo mkakati huo ulikuwa wa kipindi cha mwaka 2003-2007.

1.3 Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI

Katika kutekeleza Sera ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI, Serikali iliamua Sekta zote zishiriki katika mpango wa kudhibiti UKIMWI kwa kuanzisha Kamati za UKIMWI sehemu za kazi katika Wizara na Idara za serikali. Ofisi ya Rais, Menejimenti ya

Utumishi wa Umma ilitoa Mwongozo wa Kudhibiti UKIMWI katika Utumishi wa Umma na Waraka wa Utumishi wa Umma Na. 2 wa mwaka 2006 ulihusu jinsi ya kuwahudumia watumishi wa Umma wanaoishi na VVU na UKIMWI.

1.4 Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI Ndani ya Tume ya Utumishi wa Umma

Tume kama Idara ya Serikali ilichukua hatua ya kuunda Kamati ya UKIMWI ili kutekeleza mpango wa Kitaifa wa Kudhibiti UKIMWI. Kamati hiyo ilizinduliwa na kupewa majukumu yake katika mkutano uliofanyika tarehe 13/2/2006 hadi 17/2/2006 mkoani Arusha. Mambo mengine yafuatayo yalifanyika;

1.4.1 Tume ya Utumishi wa Umma iliandaa mafunzo kuhusu UKIMWI kwa wajumbe wa kamati ya UKIMWI ya Tume toka Makao Makuu na Kanda 7 za Kamati ya UKIMWI za Tume kwa lengo la kuwaandaa kuwa walimu wa kufundisha masuala ya UKIMWI sehemu za kazi ambapo jumla ya washiriki 41 walihudhuria mafunzo hayo. Mafunzo yaliendeshwa kwa muda wa majuma mawili kuanzia tarehe 3 – 16/1/2007.

1.4.2 Madhumuni ya mafunzo hayo kwa wajumbe wa kamati ya UKIMWI ya Tume yalikuwa ni kuwawezesha washiriki kujadili masuala ya UKIMWI, kuwaandaa

washiriki kuwa waelimishaji wa masuala ya UKIMWI na kupanga mipango ya UKIMWI sehemu za kazi.

1.4.3 Hata hivyo, katika kuhakikisha kuwa suala la UKIMWI katika Tume linapewa umuhimu unaostahili na kwamba linaungwa mkono na Menejimenti ya Tume, kiliandaliwa kikao cha siku mbili kuanzia tarehe 1-2/11/2005 huko Bagamoyo ambapo Mwenyekiti wa Tume, Makamishna, Katibu na Watendaji wengine wa Tume walipata fursa ya kujumuika kwa pamoja na kujifunza mambo mabalimbali kuhusu UKIMWI.

1.4.4 Pamoja na mafunzo hayo Kikao hicho kilipitisha Mpango Mkakati wa Tume wa kupambana na UKIMWI ndani ya Tume.

1.4.5 Tume imeendelea na jitihada za kuelimisha watumishi kuhusu masuala ya UKIMWI, na namna ya kujikinga kwa kutoa mafunzo na kusambaza kondomu katika ofisi zake za makao makuu na mikoani. Aidha Tume imeandaa machapisho mbalimbali yenye lengo la kuelimisha zikiwepo kofia, fulana na mabango.

1.5 Umuhimu wa Mwongozo Huu wa Tume

Mbali na jitihada nyingi zilizofanywa na Tume katika kupambana na maambukizi dhidi ya UKIMWI, Mwongozo huu wa Tume utaweka kwa uwazi zaidi huduma mbalimbali zinazotolewa na Tume kwa watumishi wake walioathiriwa na virusi vya UKIMWI kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI, Mwongozo wa kudhibiti UKIMWI katika Utumishi wa Umma na Waraka wa Utumishi wa Umma Na. 2 wa mwaka 2006.

2.0 MADHUMUNI

Tume ya Utumishi wa Umma imejizatiti kuhakikisha inadhibiti janga la UKIMWI. Miongoni mwa mipango yake iliyojiwekea ili kuwa na Watumishi wenye uwezo wa kutekeleza malengo na majukumu ya Tume kwa madhumuni yafuatayo:-

2.1 Utaratibu utakaoiwezesha Tume kusimamia suala la UKIMWI kwa ufanisi.

2.2 Mazingira yatakayo wawezesha Watumishi na familia zao kupima na kutambua hali ya afya zao.

2.3 Utaratibu utakaoiwezesha Tume kuwahudumia Watumishi wa Tume wanaoishi na VVU na UKIMWI kwa usiri.

2.4 Utaratibu utakaoiwezesha Tume kuwaelimisha Watumishi wa Tume wanaoishi na VVU na UKIMWI namna ya kujitunza na kujiepusha na maambukizo zaidi.

2.5 Kutoa elimu kwa Watumishi wa Tume ambao hawajapata maambukizi kujua jinsi ya kujikinga na maambukizi ya VVU na namna ya kuishi na Watumishi wenzao wanaoishi na VVU /UKIMWI.

3.0 WALENGWA

Walengwa wa mwongozo huu ni :-

3.1 Watumishi ikiwa na maana ya:

Watumishi wa Tume na familia zao.

3.2 Uongozi wa Tume ikiwa na maana ya:

Mwenyekiti na Makamishina.

3.3 Watendaji wa Tume ikiwa na maana ya

Afisa Mhasibu na Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Umma.

4.0 HUDUMA

4.1 Jinsi ya Kuleta Mabadiliko na Kutoa Huduma.

4.1.1 Kujenga Uwezo wa Tume Kuleta Mabadiliko

Tume kama taasisi nyingine za Serikali inaitaji kuwa na fikra sahihi katika kupunguza maambukizi ya VVU na kuenea kwa VVU katika Tume na kuhakikisha inakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu UKIMWI mahala pa kazi ilikuleta mababadiliko.

Tume itaweka mazingira salama kwa kuzingatia maadili ya kazi, kwa lengo la kupunguza maambukizi mapya kwa wafanyakazi wa Tume. Mazingira salama yataboreshwa iwapo Watumishi wa Tume watakuwa wanapata elimu ya UKIMWI mara kwa mara ili kujiepusha na maambukizi mapya.

4.1.2 Jinsi ya Kutoa Huduma

Ili mtumishi wa Tume aweze kupewa huduma anatakiwa kufuata hatua muhimu mbili zifuatazo:

(i) Kupima kwa hiari Virusi vya UKIMWI

(ii) Kutoa taarifa ya matokeo ya vipimo.

Afisa wa Tume anayehusika na kupatiwa taarifa/habari binafsi kutoka kwa Mtumishi kuhusu hali yake anatakiwa atunze siri kuhusu taarifa za Mtumishi ambaye anaishi na VVU au mwenye UKIMWI kwa kuzingatia Kanuni za Maadili ya Utekelezaji Katika Utumishi wa Umma Aya ya 9 (1) kwa kunukuu;

"**Watumishi wa Umma hawaruhusiwi kutoa kwa watu wasiohusika taarifa za Serikali, ama za siri au za kawaida, ambazo wamezipokea kutoka kwa watu wengine kwa kuaminiwa tu lakini bila idhini. Kwa kuzingatia utunzaji wa siri za Serikali, watumishi hawaruhusiwi pia kutoa**

taarifa za Serikali kwa watu wasihusika hata baada ya kuacha kazi katika utumishi wa umma"

Mtumishi aliyepata maambukizi atatakiwa kutoa taarifa kwa Katibu wa Tume na taarifa hiyo iambatishwe na vyeti vya hospitali alikopima.

4.2 Aina za Huduma

Huduma zitatolewa kwa Watumishi wa Tume wanaoishi na VVU na wenye UKIMWI pamoja na idadi ya wanafamilia kwa mujibu wa Waraka wa Watumishi wa Umma Na 2. wa mwaka 2006 kuhusu huduma kwa Watumishi wa Umma wanaoishi na Virusi vya UKIMWI na wenye UKIMWI.

4.2.1 Huduma ya Kupima na Ushauri

Huduma ya kupima na ushauri ni haki ya kila Mtumishi na itatolewa bure katika hospitali itakayochaguliwa. Katibu wa Tume atateua hospitali kwa ajili ya Watumishi kupima kwa hiari na kupata matibabu. Tume itafanya uhamasishaji kwa Watumishi wake kupima na kupata ushauri kuhusu afya zao. Kwa ngazi ya Idara na kila Mkoa kuwepo na Watoa Ushauri Nasaha (Counselors) ambao watachaguliwa na watumishi wa Idara/Mkoa husika.

4.2.2 Huduma ya Dawa

Tume itafuata taratibu ambazo Serikali imeweka na itaendelea kutekeleza utaratibu ambapo Watumishi wote wanaoishi na virusi vya UKIMWI watapata dawa za kupunguza makali ya virusi, hivyo huduma ya dawa hizo itatolewa bure katika hospitali ambayo itakuwa imeteuliwa au ambayo Mtumishi atapenda kwenda kuhudumiwa kwa aliyejitokeza baada ya kupimwa na kuthibitika kuwa anaishi na virusi vya UKIMWI.

Kwa wale watakao kuwa na UKIMWI na kupata magonjwa nyemelezi watafuata taratibu za Serikali zilizowekwa.

4.2.3 Huduma ya Chakula

Watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI wanahitajika kula mlo kamili kila siku ili kuboresha afya zao na kuongeza nguvu mwilini. Mlo kamili husaidia kuongeza nguvu mwilini na kumsaidia mgonjwa asipate magonjwa nyemelezi mara kwa mara. Tume itatoa huduma ya chakula kwa kutoa pesa kila mwezi, kwa kiwango atakachoweka Mtendaji Mkuu wa Tume, kwa watumishi wanaoishi na VVU na UKIMWI na pale itakapokuwa vigumu kupatikana kwa posho hiyo Katibu wa Tume atateua duka ambalo wanaoishi na

VVU na UKIMWI watakwenda kuchukuwa chakula vyenye thamani ya posho hiyo.

4.2.4 Huduma ya Usafiri

Tume itagharamia usafiri na posho kwa Mtumishi wa Tume anayesafiri kwenda hospitali kupata matibabu ya magonjwa nyemelezi, kupima kiwango cha CD4 na kupata dawa za kurefusha maisha(ARV), kwa taratibu zilizowekwa na serikali , kwenye kifungu cha J.2(a)(vi) cha Kanuni za Kudumu Utumishi wa Umma za Mwaka 1994.

4.2.5 Kazi Nyepesi (Light Duties)

Tume itajitahidi kuwapangia kazi nyepesi Watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI ili kulinda afya zao.

5.0 JINSI YA KUPUNGUZA MAAMBUKIZI YA VVU

5.1 Mafunzo

Tume itaandaa mafunzo ya uhamasishaji mara kwa mara kwa Watumishi kwa ujumla kulingana na Mwongozo wa kudhibiti UKIMWI katika Utumishi wa Umma ulivyoelekeza. Aidha, Tume itaendesha mafunzo kwa ajili ya Watoa Ushauri Nasaha wa Tume ili wapate stadi za kutoa ushauri nasaha kikamilifu.

5.2 Unyanyapaa, Ubaguzi wa Kijinsia na Haki za Binadamu.

Tume itatekeleza sera na nyaraka nyingine zilizopo zinazohusu usawa wa jinsia pamoja na kupinga unyanyapaa kwa nia ya kupambana na maambukizo ya VVU na kusimamia heshima ya Watumishi wanaoishi na VVU/UKIMWI. Tume itasimamia na kuheshimu haki za binadamu na itazingatia usawa wa kijinsia, usawa katika kazi, ushauri nasaha na matibabu na ufuatiliaji wa ukiukwaji wa haki za mtumishi na kuambukiza kwa makusudi.

5.3 Taarifa ya Maendeleo Juu ya Mapambano Dhidi ya UKIMWI

Tume itatoa taarifa za mara kwa mara kuhusu maendeleo ya afya za Watumishi na huduma kwa wanaoishi na VVU/UKIMWI kama zilivyofafanuliwa katika Waraka Na2. wa mwaka 2006, wa kuhudumia Watumishi wanaoishi na VVU na wenye UKIMWI.

Mratibu wa UKIMWI wa Tume ataratibu Taarifa za shughuli za UKIMWI katika Tume. Taarifa hizo zitasaidia kuonyesha hali halisi dhidi ya mapambano ya maambukizi ya VVU sehemu za kazi.

5.4 Watumishi wa Tume Kuhamasishwa Kujitangaza

Tume itaweke utaratibu wa kuhamasisha Watumishi wake kupima afya zao na kujitangaza kwamba wameathirika kwa lengo la kupunguza maambukizi na kuondoa unyanyapaa.

6.0 HITIMISHO

Tume itahakikishe Mwongozo huu unakuwa wazi kwa kila Mtumishi wa Tume na kuutekeleza katika mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU. Tume itapitia na kubadilisha Mwongozo huu kulingana na mabadiliko yatakayojitokeza ili uende na wakati.